**MAONI NA USHAURI KUTOKA KWA WADAU MBALIMBALI**

“Kitu kikubwa kinachoweza kumsaidia mwanafunzi kufanya vizuri darasani ni kujitambua.

Kujitambua kunaambatana moja kwa moja na kuelewa maana ya yeye kuwa darasani, kuelewa umuhimu wa kuwa na bidii darasani na kuelewa umuhimu wa wenzake darasani”

~**Abel E Kiharo**

“Ili mwanafunzi aweze kufanya vizuri ni pamoja na kuwa na nidhamu kwa kila anachokipanga, atambue kwamba anaweza kufanya vizuri zaidi ya wengine na asifanye mambo mawili kwa wakati mmoja maana mshika mawili moja humponyoka “~**Charles Kalungu**

“Mwanafunzi anapaswa kutengeneza mazingira mazuri ya kujisomea na kujifunzia. Hii inamaanisha kuwa mwitikio na utayari wa mwanafunzi humfanya mwalimu kutokuwa mchoyo. Yaani mwalimu akiona mwanafunzi amejiweka katika mazingira ya utayari humfanya mwalimu kutoa kila alichonacho ili kimsaidie mwanafunzi kufanya vizuri”.

~**Jacqueline Salmon**

“Mwanafunzi ili afanye vizuri anapaswa kwanza kuwa na nidhamu awapo darasani, Pili afanyie kazi kile anachofundishwa na mwalimu wake na mwisho asome kwa kurudia mara kwa mara kile anachofundishwa “

**~ Mwl Abbass Novatho**

“Ili mwanafunzi afaulu darasani anahitaji awe na nidhamu kwa watu wote, awe na bidii katika masomo na awe na kiu ya kufaulu na atafute vyanzo mbalimbali vya maarifa “

**~Mwl Anjesta Nathanael**

“Ili mwafunzi aweze kufanya vizuri abadilishe mtazamo juu ya nini anapaswa kufanya awapo darasani na nje ya darasa akiwa peke yake.

Mfano mwalimu anafundisha mwanafunzi anafikiria mahusiano, mpira, tamthilia, umbea na mambo yanayofanana na hayo hupoteza umakini wa mwanafunzi na mwisho hupelekea yeye kushindwa kufanya vizuri. Mwanafunzi anapaswa kujiepushe kuwaza vitu vilivyo nje ya masomo yake **“**

**~Mwl Mwoleka**

“Mwanafunzi anapaswa kuwa na ari yaani msukumo wa ndani wa kutaka kufanya vizuri. Akiwa na msukumo huo ndio utamfanya yeye kufanya vizuri na kuipenda shule”

**~Mwl Kifuta**

“Mwanafunzi ajitahidi kusoma mada zote, apitie mitihani iliyopita, abuni njia za majibu, asome kwa lengo, atulie na awe na amani wakati wa kufanya mitihani yake”

**~Mwl Erick Moses**

“Mwanafunzi apange ratiba yake, wakati wa likizo apate muda wa kutosha wa kupata masomo ya ziada na ajitahidi kuwa msikivu kwa kila mwalimu”

**~Mwl Abraham Daud Kamwela**

“Mwanafunzi ili afaulu vizuri ni muhimu ahudhurie vipindi darasani na asome vitabu maana mwalimu hatafundisha kila kitu “
**~Amani Mdewa**